Archdiocese of Arusha
wasso hospital

**HOSPITALI TEULE YA WASSO**
**S. L. P 42**
**LOLIONDO,**
Email: secretary@wasso-hospital.org

MEDICAL OFFICER INCHARGE WASSO DDH. P.O. BOX 42 LOLIONDO ARCHDIOCESE OF ARUSHA

**29 Juni,2022**

## TANGAZO LA AJIRA KATIKA HOSPITALI TEULE YA WASSO

Mganga Mfawidhi Hospitali Teule ya Wasso katika Halmashauri Ya Wilaya ya Ngorongoro kwa kushirikiana na Mkurugrenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro Kufatia kibali cha Ajira chenye **Kumb. Na. FA.10/128/01/"K"/117** Cha tarehe 15 June 2022 kutoka kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma,anawatangazia nafasi za kazi kwa watanzania wote wenye sifa ili kujaza nafasi kama zilivyoorodheshwa katika tangazo hili.

1. **Daktari Daraja II (Medical Doctor II) Nafasi 1**

SIFA ZA MWOMBAJI

Kuajiri mwenye kidato cha sita na mwenye shahada ya Udaktari kutoka Vyuo Vikuu / Vyuo vinavyotambuliwa na Serikali, waliomaliza mafunzo ya kazi "Intenship" ya muda usiopungua miezi kumi na miwili na kupata usajili kutoka Baraza la Madaktari Tanganyika (Medical Council of Tanganyika)

MAJUKUMU YA KAZI

I. Kufanya kazi za matibabu Hospitalini zinazohusiana na magonjwa mbalimbali katika fani husika
II. Kutoa na kusimamia Elimu ya Afya pamoja na kuboresha Afya ya Jamii katika Eneo lake la kazi
III. Kuchunguza , kufuatilia na kuzuia milipuko ya magonjwa
IV. Kutunza takwimu na kuzitumia kama itakavyokuwa imeelekezwa
V. Kubuni na kutayarisha mikakati ya kuinua ubora wa huduma katika fani ya Afya
VI. Kushiriki, kuhakiki na kuboresha huduma za Afya

MSHAHARA

Mshahara utalipwa kwa kuzingatia Ngazi ya Serikali sawa na **TGHS E**

## 2. Tabibu wa Meno Daraja la II (Dental Therapists II) – Nafasi 1

SIFA ZA MWOMBAJI

Kuajiriwa wahitimu wa kidato cha nne / sita wenye Stashahada ya Tabibu / Tabibu Meno ya muda wa miaka mitatu kutoka chuo kinachotambuliwa na serikali na uzoefu usiopungua miaka mitatu

MAJUKUMU YA KAZI: -

I. Kusimamia na kutathimini utekelezaji wa shughuli za Afya ya kinywa na meno
II. Kushughulikia matatizo ya ajali yanayohusu kinywa na meno
III. Kushiriki utafiti
IV. Kumshauri daktari wa kinywa na meno kuhusu masuala ya afya ya Kinywa na meno
V. Kufanya kazi zote za Tabibu wa meno
VI. Kutambua na kutibu magonjwa ya kawaida
VII. Kushiriki katika kupanga na kutekeleza huduma za afya msingi
VIII. Kuweka kumbukumbu za vifaa na zana za kutolea huduma
IX. Kuweka kumbukumbu, kuandaa na kutoa taarifa za utekelezaji

MSHAHARA

Mshahara utalipwa kwa kuzingatia ngazi ya Serikali sawa na **TGHS B**

## 3. Afisa Muuguzi Msaidizi II (Assistant Nursing Officer II) – Nafasi 1

SIFA ZA MWOMBAJI

Kuajiriwa wahitimu wa kidato cha nne/sita na wenye Stashahada (Diploma) ya uuguzi ,ya muda usiopungua miaka miwili kutoka chuo kinachotambuliwa na Serikali,waliosajiliwa na Baraza la Wauguzi na Wakunga Tanzania

MEDICAL OFFICER INCHARGE
WASSO DDH.
P.O. Box 42
LOLIONDO
ARCHDIOCESE OF ARUSHA

MAJUKUMU YA KAZI:

I. Kutoa huduma za uuguzi
II. Kukusanya takwimu muhimu za Afya
III. Kuelimisha Wagonjwa na Jamii Kuhusu Matatizo yao ya kiafya
IV. Kutoa huduma za kinga na uzazi

MSHAHARA:-

Mshahara utalipwa kwa kuzingatia ngazi ya Serikali sawa na **TGHS B**

4. **Mteknolojia Daraja la II (RADIOGRAFA) (Technologists Radiographer) Nafasi -1**

SIFA ZA MWOMBAJI

Kuajiriwa wahitimu wa kidato cha nne /sita na mwenye Stashahada katika fani ya Uteknolojia ya muda wa miaka mitatu kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali na ambao wamesajiliwa na mabaraza

MAJUKUMU YA KAZI

I. Kuwapima wagonjwa wanaelekezwa kwenye eneo lake la kazi
II. Kutunza mitambo na vifaa vya Radiolojia
III. Kukagua picha za X-Ray zilizopimwa kwa ubora na kutosheleza (Diagnosis Quality)
IV. Kutunza picha za Wagonjwa
V. Kutoa ushauri kuhusu masuala ya kazi za Radiolojia na mionzi

MSHAHARA

Mshahara utalipwa kwa kuzingatia ngazi ya Serekali saw ana **TGHS B**

5. **MUUGUZI II (NURSE II) -Nafasi 1**

SIFA ZA MWOMBAJI

Kuajiriwa wahitimu wa kidato cha nne na wenye cheti cha Uuguzi cha miaka miwili kutoka katika chuo kinachotambulika na serikali na kuandikishwa (Enrolled) na Baraza la Wauuguzi Tanzania

OFFICER IN CHARGE WASSO DDH. P. O. Box 42 LOLIONDO ARCHDIOCESE OF ARUSHA

MAJUKUMU YA KAZI

I. Kufanya kazi za kiuguzi za kuhudumia wateja katika jamii, Hospitali na sehemu zote zinapotolewa huduma za afya
II. Kusimamia na kuratibu kazi zote za wahudumu wa afya katika sehemu yake ya kazi
III. Kukusanya takwimu na kutayarisha taarifa za utendaji wake wa kazi
IV. Kutoa huduma kwa wagonjwa hospitalini
V. Kutoa ushauri nasaha
VI. kutoa huduma ya uzazi na afya ya mtoto
VII. kuelimisha wagonjwa na jamii kuhusu matatizo yao ya kiafya

MSHAHARA

Mshahara utalipwa kwa kuzingatia ngazi ya Serekali saw ana **TGHS A**

### 6. Mteknolojia Daraja la II (Health Laboratory Scientists) -Nafasi 1

SIFA ZA MWOMBAJI

Kuajiriwa wenye shahada ya sayansi ya Maabara kutoka chou kinachotambuliwa na serikali na kusajiliwa na mabaraza ya Taaluma husika

MAJUKUMU YA KAZI

I. Kufanya uchaguzi wa kimaabara (haemotology , parasitology,microbiology, immunology,Blood Group serology,Entomology,Clinical chemistry and histopathology katika maabara za afya na utafiti (research laboratories )
II. Kufundisha wanafunzi katika taasisi mbalimbali za afya , masomo yanayoendana na taaluma ya maabara
III. Kuchukua sampuli zinazoitaji utaalammaalum na sampuli kwa ajili ya uchaguzi katika maabara zingine za afya na utafiti
IV. Kuweka kumbukumbu za matokeo za vipimo katika rejesta
V. Kutunza vifaa na vitendea kazi vya maabara
VI. Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana na Elimu,uzoefu na ujuzi wake

MSHAHARA

Mshahara utalipwa kwa kuzingatia ngazi ya Serekali saw ana **TGHS C**

MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI WA NAFASI ZOTE

1. Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania
2. Waombaji wote wawe na umri wa kuanzia Miaka 18 na usiozidi miaka 45
3. Waombaji wote waambatanishe Nakala za Vyeti Vya Elimu na Taaluma kwa mujibu wa sifa ya kila kada
4. Waombaji wote waambatanishe Nakala ya NIDA
5. Waombaji waambatanishe Nakala ya Cheti cha kuzaliwa
6. Waombaji wote waambatanishe CV zao zenye anuani na nambari za wadhamini wasiopungua watatu
7. Maombi yaambatanishwe na picha mbili za rangi (passport size) zilizopigwa hivi karibuni
8. Waombaji waliosoma nje ya Nchi waambatanishe cheti cha Ulinganifu (Equivalent Certificate) kutoka Baraza la Mtihani la Tanzania
9. Result Slip,Testimonial hazitakubaliwa
10. Maombi yote yatumwe kwa njia ya Barua;

    ***Mganga Mfawidhi***
    ***P.o box 42***
    ***Loliondo.***

    **AU**

    Barua pepe:
    ***Secretary@wasso-hospital.org***

N. B. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **10 Julai 2022** saa tisa na nusu (9:30) Alasiri

Tangazo hili limetolewa na,

..................................

**Dr. Angela Meipuki**
**MGANGA MFAWIDHI**
**HOSPITALI TEULE YA WASSO**